

Uganda · Mawe · Ajira Kwa Watoto

Kuna taarifa kwamba watoto wenye umri mdogo wa hata miaka 7 wanafanya kazi katika machimbo ya mawe nchini Uganda. Watoto, hasa wavulana, wanachimba na kuvunja mawe katika mikoa 3 kati ya 4 ya Uganda. Maeneo ya wasiwasi wa kipekee kwa watoto wanaofanya kazi katika machimbo yanajumuisha mkoa wa Karamoja ulioko kaskazini mashariki na eneo la Uganda ya Kati. Ofisi ya Takwimu Uganda inakadiria kwamba wafanyakazi 2,124 wanashiriki kweye ajira rasmi katika uchimbaji wa mawe; wengi wao wanafanya kazi katika machimbo ya Uganda ya Kati. Hata hivyo, wafanyakazi wengi pia wanajulikana kuchimba mawe katika machimbo yasiyo rasmi, ya wachimbaji wadogo wadogo, wakiwemo watoto wengi. Kwa mujibu wa mashirika ya kimataifa, vyombo vya habari, na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, matukio kadhaa ya watoto wanaochimba na kuvunja mawe yameripotiwa kote nchini na hasa kabisa katika mkoa wa Karamoja ulioko kaskazini mashariki. Kazi hii inazuia watoto kuhudhuria shule. Aidha, watoto wanakumbana na makelele makubwa, vumbi, masaa mengi katika joto kali, na majeraha kutokana na vipande vya mawe vinavyoruka. Ajali zinazotokana na uchimbaji wa mawe zimesababisha upotevu wa viungo, kuvunjika kwa uti wa migongo, na upofu.